JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

# MWONGOZO WA MATUMIZI NA USIMAMIZI WA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

December, 2024

# DIBAJI

Vyama vya ushirika vimekuwa nguzo muhimu katika kuwaunganisha wananchi pamoja na kuinua uchumi wao. Pia, Vyama vya Ushirika kama nguzo ya kiuchumi vimekuwa vikikuza uchumi wa nchi na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Wanachama na wasiokuwa Wanachama, na hivyo kupunguza umasikili kwa wananchi. Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya Vyama vya Ushirika ili viweze kujiendesha kibiashara kwa lengo la kupata faida na kuinua uchumi wa wananchi. Miongoni mwa jitihada za serikali katika kuhakikisha vinakuwa imara, ilitengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Mfumo huu umeleta Mageuzi makubwa katika usimamizi kwa kuongeza uwazi, mawasiliano na ufuatiliaji wa karibu wa vyama vya ushirika. Pamoja na mafanikio haya bado kumekuwepo na chanagamoto katika vyama kutumia MUVU, huku vyama vingi vikiwa havijaweza kutumia MUVU kwa asilimia mia moja. Changamoto zilizosababisha kutokutumia MUVU ipasavyo ni pamoja na kutokuwepo elimu ya kutosha kuhusu matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), iliyosababishwa na kutokuwepo kwa mwongozo.

Utumiaji wa MUVI unahitaji Vyama vya Ushirika viwe na matumizi na usimamizi bora, sahihi na salama wa vifaa vya TEHAMA; matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA; kuboresha utoaji wa huduma za vyama kupitia vifaa, data na mifumo ya TEHAMA; Wanachama kujua umuhimu wa matumizi ya TEHAMA na namna inavyoweza kunufaisha maendeleo ya ushirika na jamii kwa ujumla; na kuwepo utaratibu wa ushirikiano kati ya wadau na/au watoa huduma wanaojihusisha na masuala ya mifumo ya TEHAMA. Kwahiyo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imeona ni muhimu kutoa Mwongozo huu ili kuongeza tija, usimamizi na utumiaji wa TEHAMA katika Vyama vya Ushirika. Mwongozo huu unaelekeza namna bora ya usimamizi na matumizi ya Vifaa na Mifumo ya TEHAMA moja kwa moja katika Vyama vya Ushirika. Naelekeza vyama vyote vya ushirika kutekeleza mwongozo huu kwa maendeleo ya Vyama vya Ushrika na taifa kwa ujumla.

Dkt Benson O. Ndiege,

**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**YALIYOMO**

DIBAJI ..... i
TAFSIRI YA MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA ..... iv
SEHEMU YA KWANZA ..... 1
1.0 UTANGULIZI ..... 1
1.1 Maelezo ya Awali ..... 1
1.2 Hali Halisi ya Matumizi ya TEHEMA kwenye Vyama vya Ushirika ..... 2
1.2.1 Matumizi ya TEHAMA ..... 2
1.2.2 Vifaa vya TEHAMA ..... 2
1.2.3 Ujuzi na Mafunzo ..... 2
1.2.4 Usimamizi wa Taarifa ..... 3
1.3 Malengo ya Mwongozo ..... 3
SEHEMU YA PILI ..... 5
2.0 UTARATIBU WA USIMAMIZI WA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI NA VIFAA VYA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA ..... 5
2.1 Utaratibu wa Kutengeza na kununua Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA ..... 5
2.2 Utaratibu wa Usimamizi na Uendeshaji wa Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA ..... 6
2.3 Usalama wa Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA ..... 7
2.4 Unganishaji wa Mifumo na Vifaa Vya TEHAMA ..... 8
2.5 Matumizi ya Tovuti na Mitandao ya Kijamii ..... 8
2.6 Matumizi na Usimamizi wa Baruapepe za Chama cha Ushirika ..... 9
SURA YA TATU ..... 11
3.0 UZINGATIAJI WA SHERIA, KANUNI, MIONGOZO NA VIWANGO VYA SERIKALI MTANDAO ..... 11
SURA YA NNE ..... 12
4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU ..... 12
4.1 Tume ya Maendeleo ya Ushirika ..... 12
4.2 TFC na SCCULT ..... 12
4.3 Vyama vya Ushirika vya Upili na Vyama Ushirika vya Msingi ..... 12
SURA YA TANO ..... 13

5.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 13
5.1 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mwongozo ........ 13
5.2 Viashiria vya kupima utekelezaji wa Mfumo wa Mrejesho ........ 13
5.3 Matumizi ya Matokeo ya taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ........ 13
KIAMBATISHO ........ 15

## TAFSIRI YA MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| **TEHAMA** | Ni kifupi cha "Teknolojia ya Habari na Mawasiliano." TEHAMA inajumuisha vifaa, programu, na mifumo inayohusiana na ukusanyaji, uhifadhi, uchakataji na usambazaji wa taarifa mbalimbali. Pia, inajumuisha vifaa kama vile kompyuta, mitandao, vifaa vya mawasiliano, na programu mbalimbali zinazowezesha mawasiliano na ushirikiano kati ya watu na watu, taasisi na taasisi, watu na taasisi, n.k. |
| **MUVU** | Ni Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika |
| **VYAMA** | Ni Vyama vya Ushirika vikiwemo Vyama vya Akiba na Mikopo Kifedha (SACCOS) na visivyo vya kifedha. |
| **Vifaa vya TEHAMA** | |
| **Mifumo ya TEHAMA** | |

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

Vyama vya Ushirika ni taasisi zinazoundwa na Wanachama kulingana na mahitaji yao ya pamoja, kama vile uchumi, kilimo, au huduma. Vyama vya Ushirika hivi vinaweza kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo hufanyika ndani ya maeneo yao. Vyama vya Ushirika vinategemea mshikamano na ushirikiano kati ya Wanachama ili kufanikisha malengo yao. Katika muktadha huu, matumizi ya TEHAMA yanasaidia Vyama vya Ushirika kukabiliana na changamoto za kiuchumi, kuboresha mawasiliano, na kutoa huduma bora kwa Wanachama**.** Katika ulimwengu wa kisasa, matumizi ya TEHAMA yamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha ufanisi wa shughuli mbalimbali, ikiwemo uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na kutoa huduma kwa haraka kwa Wanachama. Katika mazingira ya Vyama vya Ushirika, TEHAMA ina nafasi muhimu katika kuboresha ufanisi wa shughuli za maendeleo ya ushirika, kuongeza mashirikiano baina ya Wanachama na kuwasaidia kubadilishana taarifa kwa urahisi zaidi.

Matumizi ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika yataleta mabadiliko makubwa kutokana na namna Vyama vya Ushirika vinavyoendesha shughuli zao. Vyama vya Ushirika ni daraja linalowafanya Wanachama wawe na uhusiano wa karibu zaidi, kutoa huduma bora na kusimamia taarifa kwa ufanisi. Ili kuhakikisha mafanikio endelevu, ni muhimu kwa Vyama vya Ushirika kuwekeza katika TEHAMA na kuhamasisha Wanachama wao kutumia mifumo ya kidijitali pamoja na vifaa vya TEHAMA. Kwa hiyo, Mwongozo huu utasaidia vyama kukabiliana na changamoto zinazokumba Vyama vya Ushirika katika upatikanaji, uendeshaji, na matengenezo ya Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA. Kuhakikisha kwamba teknolojia inatumika kwa usahihi na inatoa thamani halisi kwa vyama na wanachama wake. Pia, kuimarisha uwezo wa vyama kutumia TEHAMA ili kuongeza uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa kiutendaji. Pamoja na

kusaidia vyama kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa vya usimamizi wa teknolojia na taarifa.

## 1.2 Hali Halisi ya Matumizi ya TEHEMA kwenye Vyama vya Ushirika

Usimamizi wa Mifumo na vifaa vya TEHAMA kwa Vyama vya Ushirika nchini Tanzania unapewa kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika kuboresha shughuli za kiuchumi, usimamizi wa mali na huduma kwa wanachama. Hali halisi kwenye Vyama ni kama ifuatavyo;

### 1.2.1 Matumizi ya TEHAMA

Vyama vya ushirika nchini Tanzania vimeanza kutambua umuhimu wa kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuboresha utendaji wao. Hata hivyo, utekelezaji wa mifumo hii bado uko nyuma katika maeneo mengi kutokana na mifumo mingi inayotumika kutokuwa ya ya kisasa au kutoratibiwa vyema, ukosefu wa rasilimali, na mifumo duni ya uuzaji wa mazao na bidhaa za wanaushirika. Hivyo, TEHAMA inaweza kusaidia katika kuunda mifumo ya ushirikiano na masoko kwa ajili ya bidhaa zao, kwahiyo, kuna umuhimu wa uwekezaji zaidi katika vifaa na teknolojia.

### 1.2.2 Vifaa vya TEHAMA

Upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya TEHAMA kama kompyuta, vifaa vya mtandao, na zana za mawasiliano ni kiunganishi muhimu katika uwezeshaji wa vyama vya ushirika. Hata hivyo, vifaa hivi vimekuwa na upungufu katika maeneo ya vijijini, ambako vyama vingi vinafanya kazi. Pia, kuna tatizo la uhifadhi na matengenezo ya vifaa hivyo, ambavyo mara nyingi vinaharibika kutokana na ukosefu wa rasilimali kwa ajili ya matengenezo.

### 1.2.3 Ujuzi na Mafunzo

Ujuzi wa watendaji wa vyama vya ushirika katika kutumia mifumo na vifaa vya TEHAMA ni wa kiwango tofauti. Wengi wao hawana ujuzi kutokana na kutokupata mafunzo ya kutosha kuhusu matumizi ya teknolojia, jambo ambalo linaweza kusababisha matumizi yasiyo ya kisasa au hata kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hata hivyo, kuna haja ya kushirikisha Mashirika ya serikali na yasiyo ya

kiserikali katika kuimarisha programu za kutoa mafunzo ya kitaalamu ili kuwapa Viongozi, Watendaji na Wanachama ujuzi unaohitajika katika matumizi ya TEHAMA.

#### 1.2.4 Usimamizi wa Taarifa

Kuna mifumo ya usimamizi inayotumika na vyama vya ushirika ambayo inajumuisha usimamizi wa fedha, utunzaji wa rekodi za wanachama, na uchambuzi wa uzalishaji. Hata hivyo, baadhi ya mifumo hii ina changamoto mbalimbali ikiwemo utendaji usio kuwa na ufanisi na kukosa uwezo wa kuungana na mifumo mingine. Hivyo, kuweka mfumo mmoja wa usimamizi na mawasiliano unaweza kusaidia kuboresha ufanisi na uwazi katika biashara za vyama vya ushirika.

Kutokana na hali halisi kwenye Vyama vya Ushirika, Mwongozo huu utasaidia kutatua changamoto hizi kwa kutoa maelekezo kuhusu matumizi na usimamizi sahihi na salama wa vifaa na mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika. Hivyo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa mwongozo huu ili kuelekeza Vyama vya Ushirika na wadau wa maendeleo ya ushirika kuhusu matumizi na usimamizi sahihi na salama wa vifaa na mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za maendeleo ya ushirika ili kuondoa changamoto zilizobainishwa.

### 1.3 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la mwongozo ni kuweka utaratibu wa matumizi bora, sahihi na salama ya vifaa, data na mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika. Malengo mahsusi ya mwongozo huu ni kama ifuatavyo:

i. Kuelekeza Vyama vya Ushirika kuhusu matumizi na usimamizi bora, sahihi na salama wa vifaa vya TEHAMA;

ii. Kuelekeza Vyama vya Ushirika kuhusu matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA;

iii. Kuboresha utoaji wa huduma za Maendeleo ya Ushirika kupitia vifaa, data na mifumo ya TEHAMA;

iv. Kuandaa Wanachama kuhusu umuhimu wa matumizi ya TEHAMA na namna inavyoweza kunufaisha maendeleo ya ushirika na jamii kwa ujumla;

**v.** Kuweka utaratibu wa ushirikiano na wadau na/au watoa huduma wanaojihusisha na masuala ya mifumo ya TEHAMA.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UTARATIBU WA USIMAMIZI WA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI NA VIFAA VYA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Vyama vya Ushirika vinapaswa kutumia Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA kwaajili ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kila siku zikiwemo utunzaji wa taarifa za wanachama, uchakataji wa taarifa za kifedha, uandaaji wa bajeti za chama, usimamizi wa masoko na mali za chama kwaajili ya kuongeza ufanisi na utendaji kazi wa Chama kwa ujumla. Katika eneo hili Vyama vya Ushirika vinapaswa kuzingatia yafuatayo katika usimamizi wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa hivyo:

### 2.1 Utaratibu wa Kutengeza na kununua Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA

i. Chama kitatakiwa kupata ushauri wa kitaalamu kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kabla ya kununua au kutengeneza Mfumo wa kielektroniki Uendeshaji wa shughuli za chama;

ii. Chama kitatakiwa kutenga bajeti kwa ajili ya Matengenezo, ununuzi, wauendeshaji na uendeshaji wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA;.

iii. Kwa vyama Kifedha (SACCOS), vinatakiwa kuwa na Mfumo wa kielektroniki kwa kuzingatia mahitaji na viwango vilivyoanishwa kwenye Nyaraka ya *Software Requirement Specification (SRS)* ya Vyama vya Ushirika wa Kifedha;

iv. Kwa vyama visivyo vya Kifedha, vinatakiwa kuwa na Mfumo wa kielektroniki kwa kuzingatia mahitaji na viwango vilivyoanishwa kwenye Nyaraka ya *Software Requirement Specification (SRS)* ya Vyama vya Ushirika wa Kifedha;

v. Chama kinatakiwa kuzingatia mahitaji na viwango vya msingi ya vifaa vya TEHAMA wakati wa kununua vifaa hivyo kama yalivyoainishwa katika ***Kiambatisho*** cha mwongozo huu.

vi. Kuhusisha wataalam wa TEHAMA katika kusaidia kuchagua Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA vinavyokidhi mahitaji ya sasa na ya baadae;

vii. Vyama vya Ushirika vinapaswa kuchagua vifaa vya TEHAMA vinavyoendana na mahitaji yao ya msingi, kama kompyuta (desktop, laptops, tablets, printer),

viii. Chama kitatakiwa kuwa na huduma ya Mtandao wa Internet ili kuweza kutumia mifumo ya Kielektroniki kwa ufasaha na urahisi (routers au access points, Bando).
ix. Chama kitatakiwa kutengeneza au kununua Mfumo kutoka kwa watoa huduma walioidhinishwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika;
x. Chama kitatakiwa kununua vifaa vya TEHAMA kutoka kwa Kampuni au Mtoa Huduma aliyesajiliwa na Taasisi husika ya Serikali yenye mamalaka hayo katika huduma husika;
xi. Kuhakikisha kuwa leseni na mikataba ya huduma za Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA inapatikana kwa gharama nafuu na inazingatia thamani ya pesa (value for money).

### 2.2 Utaratibu wa Usimamizi na Uendeshaji wa Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA

i. Chama kihakikishe kinaajiri mtaalam wa TEHAMA kwaajili ya usimamizi na uendeshaji wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA;
ii. Chama kiwe na Mpango maalum wa utaratibu wa kuhuuisha Mifumo ya TEHAMA (Software updates/Upgrade plan);
iii. Chama kiwe na Mpango maalum (Preventive Maitenance Plan (PMP) wa utaratibu wa kutengeneza vifaa vya TEHAMA kwa kila robo ya mwaka;
iv. Kutoa mafunzo kwa waajiriwa wa chama pamoja na wanachama kuhusu matumizi sahihi ya Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA.
v. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kugundua matatizo mapema na kuepuka gharama kubwa za matengenezo ya dharura.
vi. Kuwa na mpango wa dharura ya kurejesha Mfumo (Disaster Recovery Plan) ili kuhakikisha uendelevu wa huduma wakati wa majanga au matatizo makubwa ya Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA;
vii. Kuwa na mikataba ya huduma na watoa huduma wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA ili kupata msaada wa haraka na wa kitaalamu panapotokea hitilafu;

viii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa usalama wa Mifumo ya Kielektroniki ili kulinda taarifa za wanachama na Vyama dhidi ya uhalifu wa mtandaoni kwa kuzingatia Sera ya Usiri na Ulinzi wa taarifa za Vyama na Wanachama inayopatikana katika Tovuti ya Tume;

ix. Kutumia Teknolojia za kisasa kama antivirus, firewalls, na nakala rudufu (backups) za data ili kuhakikisha data na taarifa hazipotei;.

x. Kwa maeneo yenye changamoto ya Internet Chama kihakikishe kinapata Mfumo unaoweza kutumika pasipo kuwa na mtandao (offline) na baadae kufanya kuwasiliana (Synchronization) na Mfumo baada ya kupata Internet;

xi. Kwa maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa umeme Chama kihakikishe kinanunua vifaa TEHAMA vyenye uwezo wa kutunza umeme muda mrefu au kuwa na Kifaa cha umeme mbadala (Solar, backup battery, Generator)

## 2.3 Usalama wa Mifumo ya Kielektroniki na Vifaa vya TEHAMA

i. Kusitisha haraka matumizi ya akaunti ya mtendaji wa Chama cha Ushirika atakayeacha/ kuachishwa kazi, kustaafu au kufariki;

ii. Kuhakikisha kuwa Vifaa vya TEHAMA kama Simu, Vishikwambi, POS, Printer, Mizani ya Kidigitali vinawekewa ulinzi wa Kiteknolojia (PIN CODE, PASSWORD, BIOMETRIC) ili visiingilike au kutumika pasipo idhini ya Bodi ya Chama;

iii. Kuhakikisha Vifaa vya TEHAMA vya Chama vinawekewa Teknolojia ya (GPS Tracking), kwa ajili ya utambuzi na ufuatiliaji;

iv. Kuzuia matumizi ya mifumo ya TEHAMA ya Chama cha Ushirika kwa mtu asiye mwajiriwa bila kufuata utaratibu wa kupata kibali maalumu kama ilivyoelekezwa kwenye Sera ya Usiri na Ulinzi wa Taarifa za Wanachama inayopatikana katika Tovuti ya Tume;

v. Mtendaji wa Chama au Mhusika wa kuingia kwenye Mfumo wowote wa Chama atapaswa kuhifadhi na kulinda nywila (password) ili isifahamike na kunakiliwa kwa namna yoyote na mtu mwingine;

vi. Kubadilisha nywila kila baada ya miezi mitatu au mara kwa mara kwa ajili ya ulinzi na usalama wa taarifa;

vii. Chama kihakikishe kuwa Mifumo inahifadhiwa katika Server na mahali ambapo ni salama kwa ulinzi na upatikanaji wa taarifa wakati wote;

### 2.4 Unganishaji wa Mifumo na Vifaa Vya TEHAMA

Kutokana na umihimu wa kurahisisha utendaji na kuboresha taarifa katika Mifumo ni muhimu mifumo na vifaa vya TEHAMA kuweza kuwasiliana na kubadilishana taarifa. Katika eneo hili Vyama vya Ushirika na Wadau vinatakiwa kuzingatia yafuatayo;

i. Kuhakikisha Mifumo inayotengenezwa au kununuliwa ina uwezo wa kuunganishwa na kubadilishana taarifa na Mfumo wa MUVU kwa kutumia Teknolojia ya RESTFUL API;
ii. Kuhakikisha Mifumo ina uwezo wa kuwasiliana na Vifaa vya TEHAMA kama Mizani ya Kidigitali, Printer Kwa kutumia Wireless au Bluetooth
iii. Vifaa vya TEHAMA kama Tablets, POS, Simu Janja ziwe na uwezo wa kutumia programu za Android na iOS;
iv. Kuhakakisha Mifumo ya TEHAMA katika Vyama ina uwezo wa kufanya kazi katika programu za Android na iOS;
v. Kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa au kununuliwa ina uwezo wa kutumia Teknolojia inayopunguza shughuli kwa mtumiaji (kama vifaa vya Barcode Scanner, QR-Code Reader, Biometric devices);
vi. Kuhakikisha kuwa Mifumo ya TEHAMA inakidhi vigezo vya usalama katika kubadirishana taarifa kupitia kwenye Mtandao kwa kutumia Teknolojia za kiusalama kama (Data encryptions, authentication, validation and Authorisation);
vii. Baada ya kuunganisha Mfumo wa Chama na MUVU, Chama hakitoruhusiwa kusambaza taarifa ambazo si mali yake bila idhini ya Mrajis.

### 2.5 Matumizi ya Tovuti na Mitandao ya Kijamii

Chama kitatakiwa kutengeneza tovuti na kutumia mitandao ya kijamii katika mawasiliano na kujitangaza. Hivyo, Vyama vya Ushirika vinaekelezwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kuandaa tovuti za Chama cha Ushirika kwa muundo wa kurasa unaofuata mtiririko unaoshabihiana ili kuleta urahisi kwa mtumiaji kuelewa na kuvinjari kwa haraka pale anapokuwa anatafuta taarifa au huduma;
ii. Kuandaa tovuti za Chama cha Ushirika kwa lugha mbili ambazo ni Kiswahili na Kiingereza na pale inapobidi lugha zaidi ya hizi zinaweza kutumika ili kutoa taarifa na huduma kwa watumiaji mbalimbali;
iii. Tovuti itengenezwe kwa kutumia Teknolojia ya kisasa Mfano Tecknolojia ya ”*Content Management System”* ili kurahisha uhuishaji wake;
iv. Kuweka taarifa muhimu zinazoelezea muundo, mawasiliano na shughuli mbalimbali za Chama cha Ushirika zikiwemo taarifa za masoko na uwekezaji, mitaji, nk;
v. Kuhakikisha kinatumia mitandao ya kijamii ikiwemo Facebook, Instagram, Mtandao wa X, kwa ajili ya kujitangaza, kuwasiliana na wanachama na wanacnhi kwa ujumla;
vi. Chama kihakikishe taarifa zake zinahuuishwa mara kwa mara ili kutoa taarifa sahihi na kwa wakati;
vii. Kuweka sehemu ya majibu kwa maswali yanayoulizwa mara kwa mara na wanachama na wadau wengine kuhusu Chama cha Ushirika inayohusika (Frequently Asked Questions);
viii. Kubadilisha nywila za watendaji wenye dhamana ya kusimamia tovuti ya Chama cha Ushirika au kuweka taarifa kwenye tovuti pale ambapo kutakuwa na viashiria vya nywila zao kuvuja;
ix. Kutengeneza tovuti ya chama katika mfumo ambao utawezesha upatikanaji wake kwa urahisi katika vifaa vidogo vya mkononi kama vile simu janja na vishkwambi;
x. Kuzuia tovuti ya Chama cha Ushirika kutumika kutoa matangazo ya biashara binafsi au za kampuni, pasipo ruhusa ya Bodi ya Chama;

## 2.6 Matumizi na Usimamizi wa Baruapepe za Chama cha Ushirika

Kupitia baruapepe, Vyama vya Ushirika vinaweza kuboresha mchakato wa mawasiliano, kutoa taarifa kwa haraka, na kuweka rekodi za mawasiliano. Hii ni

muhimu katika kuhakikisha kuwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Chama cha Ushirika wanajua kuhusu shughuli, mikutano, na taarifa nyingine muhimu zinazohusiana na shughuli za Chama cha Ushirika. Aidha, baruapepe inaruhusu ushirikiano wa karibu kati ya Wanachama, kubadilishana taarifa na Wadau wa maendeleo ya Ushirika.

Matumizi na usimamizi wa baruapepe ni nyenzo muhimu katika maendeleo na ufanisi wa Chama cha Ushirika kwa kuwa ni daraja linalounganisha Wanachama na kusaidia kufikia malengo ya pamoja yanayokusudiwa. Hivyo, Vyama vya Ushirika vinaekelezwa kutekeleza yafuatayo:

i. Vyama vya Ushirika vinapaswa kuwa na barua pepe za taasisi (mfano kcu@ac.tz, edson.rulagirwa@kcu.ac.tz);
ii. Kutumia baruapepe za Ofisi ya Chama cha Ushirika katika shughuli za kila siku na si vinginevyo;
iii. Kutotumia baruapepe za Ofisi ya Chama cha Ushirika katika kusambaza taarifa ambazo ni kinyume na maadili;
iv. Kusambaza taarifa au kumbukumbu za Chama cha Ushirika kupitia baruapepe kwa wale tu waliokusudiwa kupokea, kusoma na kufanyia kazi taarifa au kumbukumbu hizo;
v. Kutotumia baruapepe ya Chama cha Ushirika kujisajili katika mitandao ya kijamii, kama vile Twitter, Facebook, Youtube, WhatsApp, Instagram, nk.;
vi. Kutotumia anwani za baruapepe binafsi katika mawasiliano ya shughuli za Chama cha Ushirika.

## SURA YA TATU

### 3.0 UZINGATIAJI WA SHERIA, KANUNI, MIONGOZO NA VIWANGO VYA SERIKALI MTANDAO

Pamoja na utekelezaji wa Mwongozo huu, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa wake wanaelekezwa kuzingatia kwa ukamilifu nyaraka zifuatazo:

i. Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;
ii. Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019;
iii. Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015;
iv. Sheria ya Miamala ya Kielekroni ya mwaka 2015;
v. Kanuni za Serikali Mtandao za mwaka 2020;
vi. Mwongozo wa Serikali Mtandao wa mwaka 2017;
vii. Waraka wa Utumishi Na. 5 wa mwaka 2009;
viii. Viwango vya Serikali Mtandao vya mwaka 2017; na
ix. Maelekezo mbalimbali kuhusu matumizi na usimamizi bora, sahihi na salama wa vifaa na mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika yatayokuwa yakitolewa na Tume kwa ajili ya utekelezaji.

## SURA YA NNE

## 4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

### 4.1 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

i. Kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kusimamia Matumizi na Usimamizi wa Vifaa na Mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika; na
ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo hu.

### 4.2 TFC na SCCULT

i. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kufuata maelekezo ya Mwongozo;
ii. Kutekeleza maelekezo ya mwongozo kwa ufanisi;
iii. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kutumia vifaa na mifumo ya TEHAMA;
iv. Kushirikiana na Wadau kutoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi Vifaa na Mifumo ya TEHAMA.

### 4.3 Vyama vya Ushirika vya Upili na Vyama Ushirika vya Msingi

i. Kutekeleza maelekezo ya mwongozo kwa ufanisi;
ii. Kuhakikisha Wanakuwa na Vifaa na mifumo ya TEHAMA;
iii. Kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa Wanachama kuhusu matumizi ya Vifaa na mifumo ya TEHAMA;
iv. Kuhakikisha uwekezaji wa mifumo unafanyika ili kuendesha shughuli za Chama cha Ushirika kidijitali.

**SURA YA TANO**

## 5.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 5.1 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mwongozo

Katika kuhakikisha uzingatiaji wa Mwongozo huu, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itafanya ufuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa mwongozo huu. Ufuatiliaji na tathmini utafanyika katika Vyama vya Ushirika mara moja kwa mwaka ili kubaini endapo Mwongozo unatekelezwa.

### 5.2 Viashiria vya kupima utekelezaji wa Mfumo wa Mrejesho

Tume ya Maendeleo ya Ushirika itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mwongozo huu kwa kuandaa viashiria vitakavyotumika kupima ufanisi wa utekelezaji wa Mwongozo. Viashiria hivyo vitalenga kubaini:-

i. Vyama vya Ushirika vilivyoanza kutumia mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma;
ii. Idadi ya mifumo ya TEHAMA iliyoanzishwa katika Vyama vya Ushirika;
iii. Uwezo wa mifumo ya TEHAMA iliyoanzishwa na Vyama vya Ushirika kubadilishana taarifa na mifumo mingine ikiwemo MUVU;
iv. Uzingatiwaji wa viwango vya uandaaji mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika;
v. Matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika;
vi. Uzingatiaji wa Mahitaji, uanzishwaji, matumizi na usimamizi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika.

### 5.3 Matumizi ya Matokeo ya taarifa ya ufuatiliaji na tathmini

Matokeo ya taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mwongozo yatakuwa na manufaa muhimu katika kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA katika vyama vya ushirika. Matumizi ya taarifa hizi ni pamoja na:

***i) Uzingatiaji Mwongozo***

Kubaini na kuchukua hatua dhidi ya Vyama vya Ushirika visivyozingatia mwongozo huu.

***ii) Kuboresha Utendaji***

Matokeo yatasaidia kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa katika utekelezaji wa Mifumo ya Kielektroniki na vifaa vya TEHAMA. Hii itatoa fursa ya kurekebisha na kuboresha mifumo ya usimamizi, utendaji wa kifedha, na shughuli nyingine muhimu za chama.

***iii) Kupanga Matumizi bora ya Rasilimali***

Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini itasaidia kubaini maeneo ambayo rasilimali (fedha, watu, na vifaa) zinatumiwa kwa ufanisi au siyo, na hivyo kusaidia kupanga matumizi bora ya rasilimali katika maeneo yenye changamoto au mahitaji makubwa.

***iv) Kuongeza Uwajibikaji na Uwazi***

Matokeo ya tathmini yataongeza uwazi na uwajibikaji kwa vyama vya ushirika. Vyama vitakuwa na zana ya kutathmini na kujua ni vipi wamefanikiwa au kushindwa katika utekelezaji wa mwongozo, na hivyo kutoa nafasi ya kujitathmini na kuchukua hatua za kuboresha.

***v) Kuhamasisha Ushirikiano na Washirika***

Matokeo ya tathmini yatasaidia kuvutia na kuhamasisha washirika wa maendeleo, wawekezaji, na wadau wa ndani na nje, kwa kuonyesha mafanikio yaliyopatikana na kubainisha maeneo ambayo yanaweza kuimarishwa, na hivyo kujenga ushirikiano wa muda mrefu.

## KIAMBATISHO

### A. MAHITAJI YA MSINGI (MINIMUM SPECS) KWA VIFAA VYA TEHAMA

**1. Kompyuta (Desktops, Laptops, Tablets)**

**a. Kompyuta za Mezani (Desktops):**

- **Processor :** Intel Core i3 au sawa (mfano AMD Ryzen 3).
- **RAM:** 4GB.
- **Hifadhi:** HDD 500GB au SSD 128GB.
- **Kadi ya Mtandao:** Ethernet (10/100 Mbps) na Wi-Fi (802.11n).
- **Mfumo wa Uendeshaji:** Windows 10 Home/Ubuntu 20.04 LTS.
- **Monitor:** 19-inch, HD (1366x768).

**b. Kompyuta Mpakato (Laptops):**

- **Processor:** Intel Core i3 au AMD Ryzen 3.
- **RAM:** 4GB.
- **Hifadhi:** SSD 128GB au HDD 500GB.
- **Battery Life:** Saa 4 au zaidi.
- **Mfumo wa Uendeshaji:** Windows 10 Home/Ubuntu 20.04.
- **Uzito:** Chini ya 2.5kg.

**c. Tablets:**

- **Processor:** Quad-Core Processor (mfano, MediaTek au Snapdragon).
- **RAM:** 2GB.
- **Hifadhi:** 32GB (na kadi ya SD kwa nyongeza).
- **Screen Size:** 8-inch, HD (1280x800).
- **Battery Life:** Saa 6.

---

**2. Vifaa vya Kuchapisha (Printers)**

**a. Printers za Laser:**

- **Kasi ya Uchapishaji:** 18 ppm.
- **Resolution:** 600 x 600 dpi.

- **Tray Capacity:** Karatasi 150.
- **Muunganisho:** USB.

**b. Printers za Wino (Inkjet):**

- **Resolution:** 4800 x 1200 dpi kwa uchapishaji wa rangi.
- **Kasi ya Uchapishaji:** 8 ppm kwa nyeusi, 4 ppm kwa rangi.
- **Muunganisho:** USB.

---

**3. Vifaa vya Intaneti na Mtandao**

**a. Routers:**

- **Standard:** Wi-Fi 4 (802.11n).
- **Bandas:** Single-Band (2.4GHz).
- **Port Speed:** 100 Mbps Ethernet Ports.

**b. Modems:**

- **Compatibility:** Modem inayooana na huduma ya intaneti ya eneo husika.
- **Speed:** Kasi ya 100 Mbps.

**c. Access Points (APs):**

- **Standard:** Wi-Fi 4 (802.11n).
- **Coverage Area:** 50 sqm kwa kila AP.

**d. Switches za Mtandao:**

- **Ports:** 5 Ports (10/100 Mbps).
- **Management:** Unmanaged Switch.

*Imetoloewa na*
**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**
Kuu Street, P.O. Box 201, **DODOMA**.
Telephone: +255 26 23 222456, Telefax: +255 26 23 21973
E-mail: **ushirika@ushirika.go.tz**, Website: **www.ushirika.go.tz**